**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI SIKIRARI**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2025**

**Kilimanjaro**


**Mkuu wa Shule :0769623261**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0756249125**

**Mwalimu wa Taaluma :0783960304**

**Patron: 0762425006**

**Shule ya Secondary SIKIRARI**

**S.L.P.155 SANYA JUU SIHA KILIMANJARO**


**Tarehe 24/04/2025**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P …………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SIKIRARI HALMASHAURI YA WILAYA YASIHA MKOA KILIMANJARO MWAKA 2025**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2025, tahasusi ya. ……………. Shuleya Sekondari SIKIRARI kilometa 8 kutoka mji wa BOMANG`OMBE. Usafiri wa bodaboda kutoka BOMANG'OMBE hadi shuleniTsh. 5,000/ au unaweza kupanda gari za kwenda Sanya juu hadi kituo cha kambi ya maziwa ya pili kwa nauli ya shilingi 500/= na kupanda bodaboda ya shilingi 2000/= hadi shuleni.

Ukitokea Arusha unashuka eneo linaitwa BOMANG'OMBE na kupanda bajaji ya kwenda SIKIRARI kwa nauli yaTshs 6,000/=.

**Muhula wa masomo unaanza tarehe.08/07/2025.Hivyo mwanafunzi anatakiwa kufikashuleni kuanziatarehe.07/07/2025.Mwisho wa kuripoti ni tarehe.30/07/2025**

**1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**Sare za Shule**

- **i.** Sare ya shule hii ni suruali nyeusi mbili zenye rinda na upana wa inch 17 chini na suruali khaki moja kwa ajili ya kushindia.
- ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu yasiyobana mwili
- iii. Sare ya Michezo ni bukta moja rangi ya blue na t-shirt moja rangi ya blue
- iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
- v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule
- vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
- vii. Sweta dark blue yenye **V** kifuani isiyo na maandishi au inapatikana eneo la shule kwa shilingi 10,000/=
- viii. Nguo za kushindia track suit rangi ya dark blue au inapatikana eneo la shule kwa shilingi 18,000/=
- ix. Tai rangi nyeusi
- x . Tisheti rangi ya blue yenye nembo ya shule au inapatikana shuleni kwa shilingi **15,000/=**

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

- i. Madaftari sita
- ii. **Ream (A4 Double A)** Moja (1) kwa mwaka na**Ruled** papaer 2 kwa mwaka

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. **Dissecting Kit** kwa wanafunzi wanaosoma **Biology;**
**v. Scientific Calculator;**
vi. Godoro liwe futi 2½ unene inch 3**(aje nalo mwenyewe)**
vii. Mashuka blue Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. **PCB**kwanja 1, Leki 1, sabuni ya maji lita 5,mopa 1 na hard brush 1
**xii.** **PCM**jembe 1 na mpini wake, panga 1, sabuni ya maji lita 5, mopa **1** na hard brush 1
**xiii. Koti nyeupe kwa ajili ya kufanyia majaribio maabara (Lab coat)**

**1. Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango yote iwekwe kwenye account no 40101200061 NMB Sikirari secondary School**

**2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu na nguo za nyumbani shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 2. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**ORODHA YA VITABU:**

Kutokana na uhaba wa vitabu, mzazi/mlezi anashauriwa kumnunulia mwanae vitabu vitakavyomsaidia katika rejea na mazoezi mengine kulingana na mchepuo anaosoma kwani vitabu vilivyopo havitoshelezi kila mwanafunzi kupata kitabu chake mwenyewe. Baadhi ya vitabu hivyo ni kama vifuatavyo:-

**ADVANCED MATHEMATICS.**

- Advanced Level Pure Mathematics, Fourth Edition by C. J.Tranter
- Pure Mathematics, Tanzania Institute of Education 5 and 6
- Engineering Mathematics sixth edition by K. A.STROUD
- AdvancedMathematics1-review (problems & solutions)
- AdvancedMathematics2-review (problems & solutions)
- Tie Advanced Mathematics

**BASIC APPLIEDMATHEMATICS:**

- Additional and Applied Mathematics by J. F.TALBERT
- Basic applied mathematics (BAM) by Respicius Kiiza and Lugano Mwanginde
- Basic applied mathematics review questions and solutions
- Tie Basic Applied Mathematics

**BIOLOGY**

- Biological science by D.J.Taylor
- Biology Advanced Level Secondary Schools Student's book form five and six (T.I.E)
- Biology Questions and answer
- Biology for Advancedlevel ,new understanding,4th Edition by Gleen&SusanToole
- Tie Biology

**CHEMISTRY**

- Chemistry in action (Michael Fremantro)
- Advanced chemistry by Michael Clugston,Rosalind Flemming
- Comprehensive approach toadvanced level CHEMISTRY questions with answers by Sedrick C. Magas, & Kira Ernest

- Advance chemistry-review
- Physical chemistry with General chemistry (Advanced) by Mark Daniel Hermes Daniel
- Tie Chemistry

**PHYSICS**

- Advanced levelphysics7th Edition by Nelkon and Parker
- Advanced physics by StervAdams and Jonathan Allday
- Advanced physics review
- Principle of physics by Chand
- Tie Physis

**GENERALSTUDIES**

1. Contemporary Approach for advanced level general studies notes (form 5 & 6)

**PRESIDENT OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**SIHA DISTRICT COUNCIL**

***REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION***

To be completed by a medical officer in respect of all form ones and five who join the school

**P ART A: TO THE MEDICAL OFFICER**

.....................................................................................

STUDENTFORM

NAME: ..................................................................................................

Please examine the above named person is to be admitted to secondary school education. Signature........................................................... Designation........................................................

Nameofhead ofschool.......................................

Officialstamp...................................................

**P ART B: TO BE COMPLETE BY MEDICAL OFFICER**

Blood corny (red and white)..........................................................................................................

Stool examination...........................................................................................................

T.B. test...........................................................................................................................

Eye test...........................................................................................................................

Ears............. ................................................................................................................

Chest...............................................................................................................................

Spleen.............................................................................................................................

Abdomen.........................................................................................................................

ADDITION INFORMATION (e.g. physical defeat or impairments)

.........................................................................................................................................................

.........................................................................................................................................................

.........................................................................................................................................................

Please certify that the above is fit to be admitted/ taken care in secondary school. Kind of care

........................................................................................................................................................

……………………………………………………………………………………………..

**P ART C: M EDICAL OFFICER CERTIFICATE**

I have examined the above named person and consider that *he/she* is not physically fit joining secondary education.

Doctor's name...................................................................... signature..........................................

Station........................................................................ Date..........................................................

.................................................

Official stamp

## TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

Mimi (mwanafunzi)............................................................................ umri.......................................

Jina la baba..................................................................... umri........................ Kata........................

Tarafa......................................... Wilaya............................... Namba yasimu.................................
S.L.P..........................................

Nani anakulipia michango (mzazi/mlezi) .........................................................................................

Kama ni mlezi jina.......................................................... umri........................ Kata........................

Tarafa......................................... Wilaya.................................. Namba ya simu..............................
S.L.P..........................................

Kiri kama utafuata sheria za shue
(mwanafunzi)..........................................................................................

Kiri kama utakamilisha ulipaji wa michango
(mzazi/mlezi) ..........................................................................................


Jina la mwanafunzi................................................. sahini........................... tarehe ............................

Jina la
(mzazi/mlezi) ...........................................................sahini........................tarehe............................

**NB:** Mwanafunzi anapaswa kujaza fomu ya matibabu iliyoambatishwa na amaelezo haya nakuiwasilisha shuleni siku hiyo ya kuwasili.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Jina la Mkuu wa Shule : DAUDI TITUS DAUDI**




**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0769623261**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0756249125 au 0624023675**
- **Mwandamizi Taaluma 0783960304**
- **Mwandamizi Malezi 0762425006**